

**Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya  
Mitaji na Dhamana (CMSA)**



**TANZANIA MORTGAGE REFINANCE COMPANY LIMITED ("TMRC")**

(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni ya Tanzania namba 212 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, cheti cha usajili namba 74792.)

---

**TANGAZO KWA UMMA  
MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA TMRC**

---

Tanzania Mortgage Refinance Company Limited ("TMRC") inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 20 Machi 2023 Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ilitoa idhini kwa TMRC kuza hatifungani yenye thamani ya shilingi bilioni 10 ikiwa ni toleo la nne la programu ya hatifungani yenye jumla ya shilingi billioni 120.

**MATOKEO YA MAUZO YA HATIFUNGANI YA TMRC**

Mauzo ya hatifungani ya TMRC yalifunguliwa tarehe 03 Aprili 2023 na kufungwa tarehe 24 Aprili 2023, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11.2 kimepatikana ikilinganishwa na shilingi bilioni 10 zilizotarajiwa kukusanya, sawa na mafanikio ya asilimia 112.8.

**IDHINI YA KUONGEZA KIASI**

TMRC ilipata idhini kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 10 na ongezeko la shilingi bilioni 1.2. Kufuatia kiasi kilichopatikana kufikia shilingi bilioni 11.2 ikiwa ni mafanikio ya asilimia 112.8, TMRC imechukua maombi yote ya mauzo ya hatifungani.

**MUHTASARI WA HATIFUNGANI YA TMRC**

Muhtasari wa takwimu muhimu za mauzo ni kama ifuatavyo:

Mtoaji	Tanzania Mortgage Refinance Company Limited
Maelezo	Programu ya Hatifungani za Muda wa Kati
Muda	Miaka 5
Aina ya Hatifungani	Daraja wa kwanza, isiyokuwa na dhamana, kiwango cha riba kisichobadilika
Toleo la	04
Namba ya Kumbukumbu	TMRC-FXD04/2023/05*
Tarehe ya Kutoa	03 Aprili 2023
Jumla ya kiwango kilichotolewa chenye marekebisho (TSH.)	10,000,000,000 (ikiwa na maombi ya nyongeza ya 1,280,600,000)
Jumla ya mtaji uliokusanya (TSH.)	11,280,600,000
Kiwango cha matokeo (%)	Asilimia 112.8% ya kiwango kilichopangwa kukusanya.
Jumla ya kiasi kilichokubaliwa (TSH.)	11,280,600,000
Kiwango cha riba	10.2% kwa mwaka
Bei ya Hatifungani	Ni ile iliyotangazwa
Kiwango cha chini	Shilingi 1,000,000 (na nyongeza ya mafungu ya shilingi 100,000)

Matumizi ya fedha zilizopatikana	Fedha zilizopatikana kwa mauzo ya toleo la nne zitatumika kugharamia mpango mkakati na kuimarisha zaidi mtaji wa TMRC.
----------------------------------	--

### SERA YA UGAWAJI

Kutokana na maombi zaidi kupokelewa, TMRC imeomba na kupata idhini ya CMSA:

- i. kutekeleza kiwango cha ugawaji wa hatifungani kufikia kiasi cha shilingi 11,280,600,000; na
- ii. kukubali maombi yote sahihi yaliyopokelewa. Waombaji wote watapokea asilimia mia (100%) ya maombi yao.

### MAELEZO YA ZIADA

Endapo mwombaji wa Hatifungani atahitaji ufanuzi, anashauriwa kuwasiliana na Wakala wa Soko la Hisa au TMRC kuitia [info@tmrc.co.tz](mailto:info@tmrc.co.tz) au +255 22 21510102.

### TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

Tafadhal angalia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa ofa:

Maelezo	Tarehe
Tarehe ya kutaarifiwa (kupitia baruapepe/simu)	Saa 2 asubuhi, Alhamisi, tarehe 04 Mei 2023
Tarehe ya Malipo (kwa taasisi za uwekezaji zenye sifa tu)	Saa 10 jioni, Alhamisi, tarehe 11 Mei 2023
Tarehe ya Kutoa	Jumatatu, tarehe 18 Mei 2023
Tarehe ya kuweka katika akaunti ya CDS	Siku hiyo hiyo
Tarehe ya kuorodhesha hatifungani kwenye soko la hisa	Ijumaa, tarehe 19 Mei 2023

### SHUKRANI

Menejimenti ya TMRC inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa hatifungani ya TMRC. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam (DSE); Dalali Mshauri Mkuu/Dalali Mfadili wa TMRC, Orbit Securities Co Ltd; Washauri wa Masuala ya Kisheria; Wahasibu Wakagazi wa Mahesabu; Msajili, CSD & Registry Company Limited.

Imetolewa na:

**Afisa Mtendaji Mkuu**

**Tanzania Mortgage Refinance Company Limited  
Ghorofa ya 15, Golden Jubilee (PSPF) Building, Ohio Street,  
P. O. Box 7539, Dar es Salaam, Tanzania**

**Tarehe: 04 May 2023**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.